Kikosi Kazi cha Usimamizi wa Kesi za Ulinzi wa Mtoto Lebanon

Mwongozo wa Usimamizi wa Kesi za Ulinzi wa Mtoto kutokea mbali kwa kufuatilia kupitia Simu[1] kipindi cha Covid-19

Machi 2020

Ulinzi wa Mtoto COVID -19 DropBox LINK

Kutokana na COVID-19 ufuatiliaji wa ana kwa ana unaweza usiwezekane muda wote kwa wafanyakazi wote wanaosimamia kesi za ulinzi wa mtoto wakihusisha watoto na familia zao.

Muongozo huu unadhamiria kusaidia uangalizi wa mtoto katika usimamizi wa kesi za ulinzi wa mtoto kutokea mbali, ukihusisha kanuni za msingi za ulinzi wa mtoto[2] za kuishi na kuendelezwa, kutokubaguliwa na kushirikishwa, ushiriki wa watoto, na maslahi bora ya mtoto. Unalenga:

- Jinsi gani wafanyakazi wanaosimamia kesi wanapaswa kutoa msaada kutokea mbali kwa watoto katika kesi walizo nazo ambazo zimetathminiwa kuwa katika hatari ya kati au kubwa;
- Masuala gani ya muhimu wafanyakazi wanaosimamia kesi wanapaswa kutilia maanani wakati wa kufanya mahojiano / tathmini ya maambukizi mapya yaliyopokelewa, au kupewa rufaa ambazo zinahitaji kushughulikiwa kutokea mbali, haswa kwa njia ya simu.

Mwongozo huu unalenga kuwasaidia wafanyakazi wanaoshughulika kupitia hatua za usimamizi wa kesi za ulinzi wa mtoto ya Ulinzi Mtoto (CP) katika wakati wa kukabiliana na mlipuko wa COVID-19 nchini Lebanon. Usimamizi wa kesi za Ulinzi wa mtoto, kikawaida ni mchakato wa muda mrefu ambao unaweza kuchukua miezi kadhaa kulingana mahitaji mtoto, namna yao ya kukabiliana na jambo, na mfumo wa kutoa msaada. Katika wakati wa dharura, changamoto mbalimbali zinaweza zikawakabili wafanyakazi wanaosimamia kesi za Ulinzi wa mtoto kwa kutoa msaada wa kihisia wa ana kwa ana, kwa watoto na familia zao katika kupata huduma kwa wakati. Katika hali kama hiyo, matukio mapya ya unyanyasaji wa watoto, kutelekezwa, ukatili na unyonyaji, yanaweza yakachochewa zaidi na ukosefu wa msaada wa ana kwa mtoto, pamoja na huduma zingine zinazo hitajika zaidi.

Kwa upande wa Lebanon, matatizo ya kiuchumi yanayoendelea, ukiongezea na mlipuko huu wa COVID-19, kuna uwezekano ukasababisha watoto ambao ni tayari ni wahanga wa kutelekezwa, unyanyasaji, ukatili na kutumikishwa kuwekwa katika hatari zaidi ya kufanyiwa unyanyasaji na wahusika majumbani kama wanafamilia, au katika jamii. Utoaji wa huduma za usimamizi wa kesi za ulinzi wa mtoto kutokea mbali unapaswa kuchukuliwa kama njia ya kutoa msaada katika hali za kipekee ambapo msaada wa ana kwa ana hauwezekani au haushauriwi kutokana na sababu za ulinzi na usalama ambazo zinazuia ufikiaji kama vile mlipuko wa COVID-19. Kutokana na hali ya dharura nchini Lebanon, usimamizi wa kesi kutokea mbali, ikiwa ni pamoja na msaada wa kihisia, na rufaa (kupitia simu) inaweza kuwa njia pekee ya kutoa huduma kwa watoto ambao ni rahisi kufanyiwa unyanyasaji licha ya changamoto zake nyingi, hatari, na vizuizi.

Kama msimamizi wa kesi za ulinzi wa mtoto wakati wa mlipuko wa COVID-19, ni muhimu kuendelea kutoa huduma ya usimamizi wa kesi kwa watoto katika hatari ya kati ama ya juu, ambazo tayari zipo katika kesi unazosimamia pamoja na kesi mapya. usimamizi wa kesi kutokea mbali unapendekezwa kama njia

[1] Tafadhali kumbuka kuwa nyaraka hii imetengenezwa kama sehemu ya Jitihada za mashirika mbalimbali zilizofanywa na mashirika mbalimbali yanayosimamia kesi za ulinzi wa mtoto nchini Lebanon ambayo ni pamoja na Save the Children, Himaya, IRC, UNICEF na UNHCR

[2] https://spherestandards.org/resources/minimum-standards-for-child-protection-in-humanitarian-action-cpms/

ya kipekee yaa utekelezaji kutokana na COVID-19. Miongozo hii initoa msaada kwa wafanyakazi wanaosimamia kesi za ulinzi wa mtoto katika mazingira tata ya kufanyia kazi. Katika hali ambapo mtoto yuko hatarini – Ufuatiliaji wa ana kwa ana na mamlaka husika ni wa muhimu (tafadhali soma zaidi juu ya hili hapa chini). Katika hali ambapo mtoto yupo katika hatari kubwa na kuwasiliana kwa njia ya simu haiwezekani itakuwa muhimu kwa mfanyakazi anayesimamia kesi za ulinzi wa mtoto (taasisi yake) kuangalia njia ambazo msimamizi wa kesi anaweza kumpata na kumtembelea mtoto kwa njia ya kipekee na mara chache ili kufuatilia usalama wa mtoto na kuhakikisha kuwa hawi katika hatari kubwa ya COVID-19. Tafadhali kumbuka hatua zinazo tekelezwa na serikali ya Lebanon kuzuia matembezi zinabakia za msingi kuzingatiwa na mashirika yote, japokuwa mtoto anapokuwa katika hatari kubwa, msimamizi wa kesi za ulinzi wa mtoto anapaswa kushirikiana na mamlaka husika (tafadhali tazama zaidi hapa chini)
Kwa kesi zote zilizo katika hatari ya kati ama ya juu, ni muhimu kumtembelea mtoto ana kwa ana pale inapoonekana ni salama dhidi ya COVID-19

Viwango muhimu vya kuzingatia / kufuata:

Masuala maalumu kwenye Usalama na Ulinzi wa mtoto wakati wa usimamizi wa kesi kutokea mbali: Katika hali ambapo una wasiwasi maalumu juu ya usalama wa mtoto nyumbani, tafadhali zingatia yafuatayo.

Hatua ya 1: Kupigia simu familia:

Tafadhali kumbuka kwamba watoto kwa kawaida hawana simu wao wenyewe, hasa watoto walio katika umri mdogo. Kwa hiyo, mfanyakazi anayesimamia kesi anapaswa kupiga namba ya mlezi mtu mkubwa anayeaminika.

- Msimamizi wa kesi anapaswa kumpigia mzazi / mlezi au mtu ambaye shirika lako limekuwa likifanya naye kazi na kama sehemu ya mchakato wa usimamizi wa kesi. Kimsingi, huyu lazima awe mtu mkubwa aliye salama ambaye aliwahi kushiriki katika mchakato wa usimamizi wa kesi kabla ya COVID-19 kuzuka.
- Msimamizi wa kesi anapaswa kuelezea kwa uwazi kuwa kutokana na mlipuko huu, hawezi kufika nyumbani hivyo anawasiliana na familia kupendekeza njia nyingine.
- Pitia hatua za usimamizi wa kesi[3] na hakikisha kuwa mlezi au mtu mkubwa anayeaminika anaelewa vizuri kila hatua.[4]
- Wasimamizi wa kesi za ulinzi wa mtoto wanapaswa kuelezea mwanzoni mwa mazungumzo ya simu kwamba unatarajia kutumia kati ya dakika 30 na 45, kulingana na usalama wa mtoto / familia na mahitaji yao
- Msimamizi wa kesi anapaswa kumtaarifu mlezi / mtu mkubwa anayeaminika kwamba kutokana na hali ya sasa, njia kuu ya mawasiliano kwa ajili ya kufuatilia mipango ya kesi ya mtoto itakuwa kwa njia ya simu.
- Mfanyakazi anayesimamia kesi anapaswa kumuelezea mlezi / mtu mzima anayeaminika kuwa ijapokuwa kujihusisha kwa mtu mzima mara kwa mara katika mpango wa kesi ni wa muhimu sana, ni muhimu pia kwa mtoto kuwa na nafasi ya kuzungumza na msimamizi wa kesi moja kwa moja. Msimamizi wa kesi anaweza kuelezea kuwa hili ni muhimu katika suala la kusaidia ustahimilivu wa mtoto.

Hatua ya 2: Thibitisha kuwa hali ya ulinzi na usalama ipo kuhakikisha mtoto hawi katika hali ya hatari zaidi, wakati wa kuomba ridhaa ya mtoto au ridhaa ya kuendelea kuongea na simu:

- Katika hali ambapo unahisi mtoto anasikika kuwa na wasiwasi usiendelee, na muulize mtoto kama anaweza kuwasiliana na wewe wakati atakapokuwa na muda kwa kukupigia simu, kutuma ujumbe mfupi, au njia nyingine yoyote ambayo yeye anapendelea.

---

[3] Tafadhali rejelea Mwongozo wa Pamoja wa Asasi za Usimamizi wa Kesi za Ulinzi wa Mtoto http://www.cpcnetwork.org/wp-content/uploads/2014/08/CM_guidelines_ENG_.pdf
[4] Taratibu zenye viwango vya utendaji vya Ulinzi wa mahakama za watoto nchini Lebanon
http://www.socialserviceworkforce.org/system/files/resource/files/SOP%20for%20Juvenile%20Protection%20in%20Lebanon.pdf

- Mara unapokuwa na uhakika wa kuendelea, tafadhali uliza maswali yafuatayo ili kuthibitisha hali ya ulinzi na usalama:
  - Unapendelea kuongea sasa hivi? Unakubali tuendelee na majadiliano haya sasa kwa njia ya simu? Au unapendelea tupange kufanya hivi wakati mwingine? Au unapendelea kunipigia ama kunitumia ujumbe mfupi ukiwa tayari?
  - Je, hii ni namba sahihi ya kukupigia? Au unapendelea nikupigie kupitia namba zingine?
  - Je unaongea na simu kutokea chumba ambayo kinakupa nafasi ya kuzungumza kwa ufaragha na usiri? Kama hili haliwezekani, ondoa shaka, tutalisimamia hili na naweza kukuuliza maswali ambayo unaweza kujibu NDIO au HAPANA kama itakurahisishia, ipo sawa?
- Kubaliana na mtoto nini cha kufanya katika mazingira yafuatayo:
  Kabla ya kuendelea, hebu tujadiliane juu ya baadhi ya hatua tunaweza kuzitumia endapo tutaingiliwa au ukajisikia haupo salama tena.
  - Mtu aliyeshiriki katika unyanyasaji, au mtu ambaye mtoto hana imani naye katika familia akipokea simu
  - Mtoto hajihisi salama / kuwa na ujasiri kwasababu mtu fulani anaweza kuwa anasikiliza mazungumzo na kuna haja ya kuachisha mazungumzo.
- Kukubaliana na mtoto kuhusu neno salama au kiashiria ambacho kinaweza kutumika kama hawatajihisi salama na wangependelea kutokuongea tena.
- Pia kukubaliana kuwa mtoto anaweza kubadilisha mada kama atajihisi kutokuwa salama au kusikilizwa na mtu mwingine. Msimamizi wa kesi anaweza kupendekeza kitu kirahisi kama vile kujadili juu ya hali ya hewa, muongozo wa COVID 19, au shughuli yoyote wanayofanya nyumbani nk, .. cha kubadilishia mada.
- Omba ridhaa kwa kurudia rudia:
  - Je, unajihisi salama vya kutosha kwa ajili ya mazungumzo yetu? Tafadhali fahamu kwamba ni sawa kuniambia hapana, naweza kukupigia tena wakati mwingine utakao kuwa mzuri zaidi kwako. Mimi nipo hapa kukusaidia.
  - Upo sawa kuongea sasa?
- Mara baada ya kuthibitisha kuwepo kwa usalama, kazi ya usimamizi wa kesi inaweza kutambulishwa. Ni muhimu kugusia usiri, ushiriki wa mtoto na dhana ya maslahi bora kwao.

*KUMBUKA: Kama mtoto hasikiki akifurahia mazungumzo tafadhali usiendelee na wape fursa ya kuwasiliana nawe wakati watakapo jisikia vizuri zaidi kuzungumza, unaweza kupendekeza kama ya kukupigia simu, ujumbe wa maandishi, au njia nyingine yoyote ambayo wanajihisi vizuri. Wakati wa janga la COVID-19, hii inaweza kuwa changamoto kwa mtoto anayeishi katika mazingira yenye msongamano mkubwa kama vile makazi yasiyo rasmi ya mahema, ambapo mtoto anakabiliwa vizuizi vya kutoka nje. Katika mazingira kama haya, ni muhimu kwamba mfanyakazi anayesimamia kesi za ulinzi wa mtoto kutumia uelewa wake wa hali ya maisha mtoto kutoka kwenye ziara alizowahi kufanya nyumbani ili kufahamu kama inawezakana ama haiwezekani kwa mtoto kupata muda na mahali salama ambapo wataweza kuzungumza kwa uhuru zaidi. Kuto kudhuru ni msingi katika hili.

Hatua ya 3: Wafuatilie familia na mtoto

- Kulingana na wasiwasi mkuu ya mtoto, kubaliana juu ya mipango sahihi ya malezi pale ambapo mtoto / au mtu mkubwa atakapougua.
- Msimamizi wa kesi anapaswa kuliwezesha hili kwa mtoto kwa kuelezea kwa mtu katika familia, kwamba inapendekezwa kwa mtoto kwenda katika chumba peke yake na kuzungumza kwa faragha ikiwezekana. Wasimamizi wa kesi wanapaswa kuelezea kwamba sote tunapaswa kuzingatia miongozo ya Serikali ya Lebanon (Gol) ya kuacha matembezi, waombe kukaa karibu na nyumbani kwao iwezekanavyo kuzungumza kwa faragha ili kuenda sambamba na maelekezo ya serikali ya kuzuia misongamano.
  ** Tafadhali kumbuka ni jukumu la wafanyakazi wanaosimamia kesi kuzingatia matatizo yoyote yanayoweza kujitokeza katika suala la mtoto kuwa na nafasi na muda wa kuzungumza na msimamizi wa kesi bila kuingiliwa na mtu mkubwa, au mwanafamilia mwingine.*
  ** Tafadhali kumbuka kwamba watoto waaoishi katika mazingira ya msongamano mkubwa kama vile makazi ya mahema, watoto hawawezi kuwa na fursa ya kwenda chumba tofauti. Katika hali kama hizi msimamizi wa kesi anahitaji kuuliza maswali ya ndio au hapana ikiwa mtoto hajisikii vizuri*

kuzungumza baadhi ya mambo kupitia simu. Katika hali kama hizi wasimamizi wa kesi wanapaswa kumuelezea mtoto kuwa ijapokuwa hawaruhusiwi kutoka nje, kama kuna eneo la nje, nje ya nyumba yao, karibu na hema lao ambapo wanaweza kuwa na nafasi ya kuzungumza (bila ya kukutana na mtu yeyote), unaweza kupiga tena wakati wanaweza kuzungumza.

- Kwa wasio na wazazi, na watoto waliotengwa hakikisha unazingatia njia mbalimbali za mipango ya malezi, hakikisha familia wanayoishi nao inawachukulia kama watoto wengine katika familia.
- Mpe mtoto, pamoja na mlezi (inapohitajika) habari za mara kwa mara juu ya huduma zinazopatikana na kuweza kufikika wakati wa dharura katika
- maeneo yao ambazo zitamuhudumia mahitaji yake na ya familia yake.
- Kufanya rufaa za muhimu pale inapohitajika na kusimamia matarajio kuhusu utoaji wa huduma kutokana na hali ya sasa kusisitiza kuwa ucheleweshaji unaweza kutokea.
- Kuhakikisha kuwa majadiliano yako na mtoto na mlezi yanahusisha kuyapa vipaumbele mahitaji ya dharura ambayo yanapaswa kushughulikiwa kwa haraka, n ani rufaa zipi za lazima za kupewa kipaumbele.
- Kuwajulisha watoto na walezi juu ya msaada wa Afya ya Akili (MHPSS)[5] namba ya simu ya dharura (EMBRACE[6]: 1564) kama wanahitaji msaada wa kihisia ukiwaelezea kuwa msaada wa kihisia, na msaada ni kawaida.
- Mjulishe mlezi juu ya maombi ya MHPSS HATUA KWA HATUA[7] mpango wa kujihudumia unaopatikana kwa watu wa mataifa yote (Lebanon, Palestina na Syria) ambao unatoa msaada wa kisaikolojia na kijamii kupitia programu ya simu (taarifa za mawasiliano zinapatikana hapa chini na kwenye jedwali hapa chini). Endeleza mfumo unaomlenga mtoto, kuhakikisha kuwa maslahi bora ya mtoto ndio katika msingi wa mipango ya kesi Kuhakikisha kwamba mtoto anahusishwa vyema katika kufanya maamuzi katika mchakato mzima wa usimamizi wa kesi, ili ieleweke kwa nini na kwa jinsi maamuzi yalichukuliwa kama sehemu ya mpango wa kesi yao.

Vitu mahususi vya kuzingatia

Masuala mahsusi katika matukio ambapo mtoto, au mlezi analia kwenye simu:

Msimamizi wa kesi za ulinzi wa mtoto lazima azingatie **kauli zenye kuleta nafuu** na kuhalalisha hisia za mtoto au mtu mkubwa. Hii inamaanisha kurudia rudia kauli kama "Ni lazima kuwa ngumu, nina uhakika haikuwa / si rahisi kupitia haya yote".

Masuala mahsusi katika matukio ambapo mtoto, au mlezi anakueleza kwamba wanasumbuliwa na dalili za COVID19:

Hakikisha unamwambia mtoto na mlezi / mtu mkubwa anayeaminika kama wanaona dalili yoyote COVID19 (joto la mwili kupanda, kukohoa, matatizo katika upumuaji, maumivu ya koo, uchovu, kuhara, kutapika, mafua) au wanamtunza mtu yeyote anaye onyesha dalili hizi au alikuwa na amekutana na mtu yeyote aliyesafiri nchi za nje, tafadhali wapige simu Wizara ya Afya ya Umma kupitia namba maalumu ya COVD-19 **76-592699** / **140 (Shirika la Msalaba Mwekundu Lebanon)** / **01380000 (Rafik El Harriri Hospital).**

---

[5] https://www.moph.gov.lb/en/Pages/6/553/the-national-mental-health-program

[6] https://embracelebanon.org/

[7] **Hatua- kwa hatua za maombi**: **Hatua- kwa hatua za maombi ya MHPSS** ni msaada binafsi, unaojikita katika hadithi7, ufumbuzi unaohitaji uelekezi kidogo, iliyozinduliwa na Programu ya Taifa ya Afya ya Akili katika Wizara ya Afya ya Umma nchini Lebanon na Shirika la Afya Duniani. Ufumbuzi huu ulitumika katika mazingira ya kawaida kupitia njia ya ushirikishwaji ukihusisha makundi makuu yaliyopo nchini Lebanon: Walebanon, Wasyria na Wapalestina.
Zilizopo hapa chini ni viungo unapoweza kupakua maombi / tovuti
Tovuti: khoutouwat.com
Apple Store: https://apple.co/38zurWl
Playstore:https://bit.ly/2LNK4Qk

Masuala maalum kwa watoto wanaokaribia kuwa hatarini:

- Kwa watoto walio hatarini, haswa nyakati ambazo kutembeleana nyumbani haiwezekani tena - hakikisha rufaa ya haraka imetolewa na imefanyiwa kazi. Hii inahusisha uratibu wa karibu na mwendesha mashtaka mkuu kupitia Umoja[8] kwa ulinzi wa mahakama za watoto nchini Lebanon (UPEL) na katika kesi ya Lebanon kaskazini tafadhali fanya uratibu na Himaya[9] sambamba na SOPs za kitaifa[10]. Tafadhali kumbuka pia Mwendesha Mashitaka pia anapatikana kwa njia ya simu kama kuna dharura.
- Katika tukio ambapo mzazi / mlezi anamweka mtoto hatarini, fikiria kuangalia na mtoto kama kuna mtu mwingine nyumbani au katika maeneo ya karibu anayeaminika.
- Katika hali za dharura ambapo mtoto yuko hatarini ambapo msimamizi wa kesi atahitaji kufanya kutembelea nyumbani mfanyakazi anayesimamia kesi atapaswa kufuata tahadhari zote muhimu kama ilivyoelezwa katika "*Mwongozo kwa ajili ya wafanyakazi wanao simamia kesi za Ulinzi wa Mtoto Watoto kuwashirikisha watoto au Walezi juu hatua za usalama za kujikinga na COVID-19 wakati wakifanya usimamizi wa kesi*" Iliyoandaliwa na Kikundi kazi cha kitaifa cha usimamizi wa kesi nchini Lebanon "

Vitu vya msingi vya kuzingatia katika kesi mpya:

- Kama mfanyakazi anayesimamia kesi za ulinzi wa mtoto atapokea simu kutoka mtoto au mtu mwigine kuripoti unyanyasaji, ukatili, utumikishwaji au kutelekezwa, mtendaji wa kuwalinda watoto ana wajibu wa kulishughulikia.
- Wafanyakazi wanaosimamia kesi za ulinzi wa mtoto wanapaswa kumhakikishia mpigaji awe ni mtoto ama mtu mwingine kwamba kesi yake itakuwa ikishughulikiwa na shirika lingine (kutoa maelezo mengi iwezekanavyo kuhusu shirika na mtu wa kuwasiliana naye kadri tuwezavyo ili kumuhakikishia usalama mtoto). * Toa tu taarifa zilizothibitishwa na eleza kwamba kama shirika hili halitamuhudumia kwa sababu yeyote ile / utabakia kuwa mtu wa kuwasilina naye.
- Kama mtu mwigine anapiga simu, mfanyakazi anayesimamia kesi anapaswa kumfanyia tathimini mpigaji ni kwa kiasi gani mtoto atakuwa katika hatari na ikiwa mtendaji wa ulinzi wa mtoto aliwahi kujaribu kumfikia mtoto kwa simu- aidha kwa kupigia mwaafamilia zao, au mtu mwingine anayehusika nyumbani / katika jamii.
- Mpango wa usalama umewekwa na mtoto anayehusika na / au familia mpaka watakapo wasiliana na shirika lingine la usimamizi wa kesi za ulinzi wa mtoto.

Majukumu ya wasimamizi wa kesi za ulinzi wa Watoto:

- Hakikisha namba mahususi za kupiga simu zinapatikana wakati wote, na ziwe na salio la kutosha.
- Hakikisha mtoto na familia wana namba muhimu za kuwasiliana na wewe, ikiwa ni pamoja na namba ya kutoa huduma iliyo hewani saa 24 na namba ya kuwasiliana moja na msimamizi wa kesi.
- Kama wasimamizi wa kesi wanafanya kazi kutokea nyumbani, wanahitaji kupata chumba / sehemu salama yenye usiri ya kufanyia ushauri kwa kuheshimu faragha ya mtoto.
- Kuwa tayari kwa ajili ya dharura na uwe na habari za mara kwa mara juu ya madaktari waaofanya uchunguzi katika eneo hilo, sehemu na mawasiliano ya watoa huduma za vipimo vya kitaalamu, huduma kwa wahanga wa ubakaji, mawasiliano na Shirika la Msalaba Mwekundu kwa ajili ya kuripoti hali inayo hatarisha maisha au dalili za Covid-19 au unapokuwa umejitenga nyumani na kushindwa kufikia huduma.

---

[8] http://www.upel.org/
[9] https://www.himaya.org/
[10] http://www.socialserviceworkforce.org/system/files/resource/files/SOP%20for%20Juvenile%20Protection%20in%20Lebanon.pdf

- Kama kuna dharura inayohusiana na kesi ya hatari na mtoto yuko hatarini mfanyakazi anayesimamia kesi za ulinzi wa mtoto anapaswa kuwasiliana na kiongozi wake wa usimamizi wa kesi za Ulinzi wa Mtoto.
- Kuwajulisha UPEL (Kusini, Bekaa na Mlima Lebanon / Beirut) na Himaya (Kaskazini) katika matukio ambapo kesi ya mtoto inahitaji ya kufikishwa kwa hakimu wa mahakama ya watoto au mwendesha mashtaka mkuu. Tafadhali kumbuka wafanyakazi waaosimamia kesi bado wanawajibu wa kufuatilia na kuhakikisha mtoto anapata msaada muhimu.
- Wafanyakazi waaosimamia kesi za ulinzi wa watoto wanawajibu wa kuangalia mara kwa mara huduma za ramani mtandaoni kubaini huduma zinazoongezwa kwa ajili ya mtoto na familia. Iwapo msimamizi wa kesi hajabaini huduma yeyote husika katika jamii- Mratibu wa CPWG au mhusika wa UNHCR CP / GBV anaweza kutoa msaada wa ziada kubaini huduma za ziada.

Njia ya Kufuatilia:

Je msimamizi wa kesi anaweza kupiga simu kwa familia ya mtoto na mtoto?

Ndio

Msimamizi wa kesi atazungumza na mtoto na kuuliza yafuatayo:
Unaweza kwenda kwenye chumba kingine / kuwa peke yako ukizungumza kwenye simu? Je, unajihisi salama kufanya hivyi?

Ndiyo

Endelea kufuata miongozo ya mazungumzo kwa njia ya simu hapa chini.

Tathmini wakati wa mazungumzo: mtoto yupo salama?

Ndiyo

Unda mpango na mtoto na fanya mazoezi ya jinsi mtoto ataweza kujibu kama atajihisi hayuko salama. Atafanya kitu gani? Atasema nini? Ni muhimu kwa watoto kujifunza kusema "hapana!" na mtu mzima ambaye anafanya kitu chochote ili kuwafanya wasijihisi vizuri.

Hapana

Mtoto yupo salama?

Ndiyo

Msimamizi wa kesi anapaswa kupanga muda mwingine wa kuzungumza na mtoto wakati atakapoweza kuwa peke yake / kujihisi salama kuzungumza na simu.

Hapana

Je mhusika yupo ndani ya nyumba?

Hapana

Mtulize mtoto a umshauri kuendelea kukaa ndani ya nyumba ili kuepuka kukutana na muhusika wakati mpango wa kushughulikia kesi unaendelea kutekelezwa.

Ndiyo

Hapana

Je mtoto yupo katika hatari?

Hapana

Itisha mkutano wa haraka wa kushughulikia kesi na shirika linanotambulika na linaloweza kumfikia mtoto ili kuweka mikakati bora na ya haraka ya kuingilia kati.

Ndi

Hapana

Je mtoto anaweza kutupatia namba ya mtu mkubwa salama ambao yeye anamwamini (kama ni jamaa, jirani, au mtu katika jamii ambayo mtoto anamwamini)?

Ndiyo

Mpigie simu na kupanga kikao cha kufuatilia na kuchukua hatua muhimu kulingana na itifaki za usimamizi wa kesi. (Mfanyakazi wa kesi anaweza kujadili / kupitia upya mpango wa usalama na “mtu mkubwa wa kuaminika” mpya).

Muhakikishie mtu mkubwa salama kwamba tunapatikana muda wowote ule kwa masuala ya haraka kumhusu mtoto.

Itisha mkutano wa haraka wa kushughulikia kesi na shirika linanotambulika na linaloweza kumfikia mtoto ili kuweka mikakati bora na ya haraka ya kuingilia kati.

Toa rufaa kwenda kwa Mwendesha Mashitaka Mkuu / UPEL / Himaya

Mwongozo wa maongezi kwa njia ya simu: Wakati ukipiga simu kufuatilia kesi mpya kwa mara ya kwanza

ELEZEA mtoto na mlezi wewe ni nani, unafanya kazi na shirika gani na jinsi gani unaweza kumsaidia.

ELEWA sababu gani mtoto amekupigia au ameelekezwa kwako, hali aliyo nayo kwa sasa na ni kitu gani anategemea kutoka kwako.

ELEZEA mtoto kwamba kwa sababu ya hali iliyopo sasa, sisi, wafanyakazi wanaoshughulikia kesi hatuna uwezo wa kuja kuwatembelea nyumbani kwao mara kwa mara kama ilivyokuwa hapo mwanzoni, lakini badala yake tunaweza kuwa na mazungumzo kwa njia ya simu. Hakikisha kuwa mtoto anapendelea wazo hili.

Mwulize mtoto na mlezi iwapo wanapokea msaada kutoka kwa asasi nyingine yoyote? Fikiria kama kuna marudio yoyote, kama hakuna basi endelea kutoa huduma. Kama yapo muulize mtoto / mlezi kufikiria yupi kati ya wafanyakazi wawili wanaosimamia kesi za ulinzi wa mtoto angependa kuendelea naye.

UJUMBE MFUPI UNAOWEZA KUTUMIA: Katika wakati huu NGO's (kama vile ,weka jina la shirika lako) zote zinajaribu kufuata mapendekezo ya kubakia ndani ya nyumba na kuzuia mizunguko yote. Sababu ya sisi kuambiwa kufanya hivyo ni kuzuia kuenea kwa virusi viitwavyo COVID-19 ili kuwalinda watu wengi waliodhaifu kupambana na virusi hivyo kama vile wazee. Kama hatutatoka nje virusi haviwezi kusambaa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine na tutakuwa tumejiepusha kuvipata.

MHAKIKISHIE mtoto kwamba bado tunaendelea kumsaidia kwa kila msaada atakaouhitaji.

Unapopiga simu kwa ajili ya ufuatiliaji wa kesi.

ELEZEA mtoto lengo la kumpigia simu na kwamba mfanyakazi anayesimamia kesi atakuwa akimuuliza maswali kadhaa kuona jinsi anavyojihisi na nini kinachofanyika kwa sasa.

ELEZEA mtoto kwamba anapaswa tu kukubali kuzungumza / kujibu maswali pale anapojihisi salama kabisa na hana hofu ya athari kulingana na mazungumzo haya kwa njia ya simu.

MKUMBUSHE mtoto "neno la usalama" ambalo mlikubaliana awali (wakati wa mipango ya usalama) na kwamba anaweza kulitumia wakati wowote wanaohitaji msaada zaidi au kama atajihisi kutokuwa salama katika hatua yoyote wakati wa mazungumzo na mfanyakazi anayeshughulikia kesi. Kama hamkukubaliana juu ya "neno la usalama" na mtoto hapo awali, kubaliana naye wakati wa mazungumzo huku ukimuelezea madhumuni ya neno hili na jinsi anavyoweza kulitumia.

MUULIZE MTOTO:

Rejelea kidogo kutoka kwenye kipindi kilichopita na kuendeleza msingi wa ufumbuzi kutokea kwenye mpango wa usalama uliokwisha anzishwa; Unakumbuka mpango wa usalama tuliouweka pamoja (kulizungumzia hilo na mtoto kupitia simu)? Je, kuna taarifa yoyote ungependa kuishirikisha leo?

Jinsi mambo yalivyoendelea tangu mazugumzo yetu ya mwisho? Je anakabiliwa na kiwango kile kile cha hatari? Cha Juu? Cha Chini? Kuna kitu kilichotokea tangu mazugumzo ya mwisho ambayo mtoto anataka kumshirikisha mfanyakazi anayesimamia kesi?

Unataka tukubaliane juu ya neno la usalama ambalo linaweza kutumika wakati wowote ambao hujisikii salama au hauwezi kufanya majadiliano (kama hamkuwahi kufanya hivyo kabla)?

MUULIZE MTOTO:

Anajisikiaje? Unajihisi uko salama?

KUTAFITI NA MTOTO madhara mengine (mapya) hasi yatokanayo na COVID-19 ambayo atakuwa akiyapitia, na jinsi yanavyomfaya ajisikie?

Mfano; Kushindwa kuhudhuria shule? Kutoweza kuhudhuria shughuli za PSS? Hawaruhusiwi kwenda nje? Amepitia hatari zingine (kama mvutano katika nyumba? Kuongezeka kwa mbinu hasi za kukabiliana nao - aina mbaya zaidi za ajira kwa watoto, unyanyasaji wa ndani baina ya wapenzi na unyanyasaji wa majumbani, kuogezeka kwa viwago vya msongo wa mawazo na mvutano? Kuongeza vurugu nyumbani? Unyanyapaa? Kumpoteza a mlezi / mtu katika familia? Kutengwa na mlezi kutokana na wao kulazwa hospitalini nk?

Jadili kama mtoto na familia / walezi wameweza kupata sabuni, kama sio wasiliana na mhusika wa CPWG kupata kufahamu njia mpya za huduma za maji a usafi na kuomba nyenzo za usafi.
MUULIZE MTOTO hali yake ipoje na kama ana dalili zozote za COVID 19?
Kutoa mafunzo kidogo kumuelimisha au kumkumbusha mtoto kuhusu hatua za kujikinga na COVID-19 ili kuimarisha ujumbe unaotolewa na vituo vingine au vipindi cha muda mrefu kama mtoto bado hajapokea ujumbe wowote. "Tafadhali rejelea kumbukumbu ya muongozo kwa wasimamizi wa kesi za ulinzi wa mtoto kufanya vipindi vya uelimishaji ili kuwasaidia watoto kufahamu COVID-19 na jinsi ya kuijadili"
MUULIZE MTOTO jinsi mtoto anavyo shirikiana na watoto wengine? Ni shughuli zipi za kila siku wanazozifanya? Muulize mtoto kuhusu ustawi wake wa kisaikolojia / muulize mtoto kuhusu familia yake na watu wake wa karibu. Muulize mtoto kama anajihisi salama ndani ya utaratibu aliopo wa malezi na mazingira. Anahitaji nini kujihisi salama? Ni hatua gani kuu ambazo tunaweza kuchukua kumsaidia?
KUTOA mfanyakazi anayesimamia kesi anapaswa kumkumbusha mtoto namba ya dharura na namba ya mfanyakazi anayesimamia kesi na kumuhimiza ampigie muda wowote atakapo muhitaji.

Pale ambapo mtoto au familia inatumia Whatsapp tu, mfanyikazi wa kesi anapaswa kuwasiliana kupitia WhatsApp. Mtoto anaweza kuombwa kutuma ujumbe wa maandishi au kwa kujaribu kumpigia msimamizi wa kesi naye atampigia tena. Mpango wa usalama uliotengenezwa hapo awali utakuwa ulihusisha maelezo haya na mbinu za mawasiliano.

KILA WAKATI: Mjulishe mtoto kutoa maoni kwa uhuru na kuzungumza kama anavyotaka. Tumia mawasiliano chanya na ujuzi wa kusikiliza. Kuwa makini na mwenye ujuzi, kuwa muangalifu na mwenye utayari, kujiamini!

- Wasimamizi wa kesi za mtoto wanapaswa kufanya kazi na mtoto katika mzunguko wenye usalama kwake na kuhakikisha kuna mpango wa usalama kuhusu usalama wao kimwili na usalama wao katika mpango wa malezi pale mwanafamilia atakapokuwa ni mgonjwa wa COVID-19.
- Kuhakikisha mpango wa usalama unauhalisia na unafuata mapendekezo ya mtoto / mlezi kulingana na uwezekano.

KUMSAIDIA MLEZI

Ingawa mwongozo huu unalenga katika kazi za msimamizi wa kesi na mtoto, itakuwa muhimu pia kuangalia jinsi walezi wanajihisi. Katika hali hii maalumu, walezi wanaweza kuhisi kuzidiwa, hofu, wasiwasi, kukosa nguvu, kuchanganyikiwa na uwezo wao kimalezi. Kadri hali ya wasiwasi inavyozidi kuongezeka katika kaya, unyanyasaji wa majumbani, adhabu ya viboko na aina nyingine za unyanyasaji dhidi ya watoto na njia hasi za kukabiliana na mambo pia huongezeka.

1. Tafadhali rejelea “Mwongozo kwa wafanyakazi waaosimamia kesi za Kulinda Watoto juu ya Jinsi gani Walezi wanaweza kusaidia watoto wakati wa COVID-19, iliyoandaliwa na Kikundi Kazi cha Kitaifa cha usimamizi wa kesi"
2. Zingatia kuwaelekeza kwenye vikao vya pamoja vya walezi kutoka kwenye program ya malezi ambayo inaelezea jinsi ya kukabiliana na msongo, na nidhamu chanya.
3. Zingatia kuwafahamisha namba maalumu ya kutoa usaidizi kwa watoto na walezi ambao wanahitaji msaada wa kihisia au wanafikiria kujiua.
4. Zingatia na washirikishe Hatua kwa- hatua za Maombi: Hatua- kwa hatua za maombi ya MHPSS ni msaada binafsi, unaojikita katika hadithi, ufumbuzi unaohitaji uelekezi kidogo, iliyozinduliwa na Programu ya Taifa ya Afya ya Akili katika Wizara ya Afya ya Umma nchini Lebanon na Shirika la Afya Duniani. Ufumbuzi huu ulitumika katika mazingira ya kawaida kupitia njia ya ushirikishwaji ukihusisha makundi makuu yaliyopo nchini Lebanon: Walebanon, Wasyria na Wapalestina.
   Zilizopo hapa chini ni viungo unapoweza kupakua maombi / tovuti

Tovuti: khoutouwat.com
Apple Store: https://apple.co/38zurWl
Playstore: https://bit.ly/2LNK4Qk

Ulinzi na Usalama wa Data

Kama wafanyakazi wanaosimamia kesi za ulinzi wa mtoto watajaza fomu yeyote wakati wa mazungumzo, ni muhimu kuhakikisha uhifadhi salama wa taarifa yoyote inayomtambulisha ya mtoto. Nyaraka zilizoandaliwa wakati wa usimamizi wa kesi kutokea mbali zinapaswa kutunzwa kwa njia sawa na zile za usimamizi wa kesi wa ana kwa ana. Katika hali kama hizo, tafadhali weka taarifa katika mahali salama panapofungwa. Kama kuna mfumo wowote wa kielektroniki wa usimamizi kesi (kama vile PRIMERO), tafadhali fuata makubaliano ya awali ya hatua za usalama wa data.

Tafadhali kumbuka pale utakapohitaji mwongozo wa ziada kwa ajili ya wafanyakazi wanaosimamia kesi za ulinzi wa mtoto, tafadhali toa taarifa kwa kiongozi wa kikundi kazi cha kitaifa cha usimamizi wa kesi:
Sara.mabger@rescue.org
Monica.Martinez@savethechildren.org
Au kiongozi wa kikundi kazi cha Ulinzi wa watoto katika Dharura:
jatwi@unicef.org